# WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL

Namba ya usajili wa shule S. 3560

Namba ya usajili wa mtihani: S4014

P.O.BOX 11064
ARUSHA – TANZANIA
Executive Chairman: +255754 - 421042
Managing Director: +255754 - 381844
School Director: +255754 - 646446
HOS phone: +255766 - 657959
Bursar phone: +255745 - 6579-59
Email:winningspirit547@yahoo.com
info@winningspirithighschool.com
www.winningspirithighschool.com

**JOINING INSTRUTION**
**FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2026/2027**

**Ndugu Mzazi / Mlezi wa ………………………………………………..……….**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa Mwanao amechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha………………………………… Mwaka……………………………….……

Anatakiwa afike shuleni tarehe………………………………………………………

**Tarehe ya kufungua shule ni tarehe 07/01/2026.**

**MAELEZO KUHUSU SHULE.**

Shule ya Sekondari Winning Spirit ipo Campus ya Terrat – Arusha , umbali wa mita 800 kutoka barabara ya East Africa.

Shule inaongozwa na bodi huru ya shule. Imeandikishwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na Inasomesha masomo ya kawaida ya Sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha Sita, pia ina mchepuo wa masomo ya biashara. Ni shule ya mchanganyiko Wavulana na Wasichana, ni ya bweni (Boarding school).

1. **ADA NA MICHANGO YOTE YA SHULE:**
**MWANAFUNZI WA BWENI KWA MWAKA**

**a) Ada kwa mwaka ni shillingi 1,850,000/=**

| ADA KIDATO CHA KWANZA NA CHA TATU | ADA KIDATO CHA PILI NA CHA NNE |
|---|---|
| **i.** Awamu ya kwanza **January 462,500/=** | **i.** Awamu ya kwanza **January 462,500/=** |
| **ii.** Awamu ya pili **April 462,500/=** | **ii.** Awamu ya pili **April 662,500/=** |
| **iii.** Awamu ya tatu **July 462,500/=** | **iii.** Awamu ya tatu **July 725,000/=** |
| **iv.** Awamu ya nne **September 462,500/=** | |

**b) Michango ni kama ifuatavyo;**

| | I | II | III | IV |
|---|---|---|---|---|
| Kiingilio kwa mgeni | 150,000 | 150,000 | 150,000 | 150,000 |
| Huduma ya kwanza | 70,000 | 70,000 | 70,000 | 70,000 |
| Tahadhari | 70,000 | 70,000 | 70,000 | 70,000 |
| Mtihani(mock,pre nation,necta) | - | 250,000 | - | 300,000 |
| Computer lab service | 70,000 | 70,000 | 70,000 | 70,000 |
| Mahafali | 60,000 | 60,000 | 60,000 | 150,000 |
| Michezo | 70,000 | 70,000 | 70,000 | 70,000 |
| Uniform | 370,000 | 370,000 | 370,000 | 370,000 |
| Maabara (practical) | 60,000 | 60,000 | 100,000 | 100,000 |
| Kitambulisho | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| **TOTAL** | **930,000/=** | **1,180,000/=** | **970,000/=** | **1,360,000/=** |

2. **SARE ZA SHULE, ZINAPATIKANA SHULENI**
**WAVULANA**

- SURUALI 2
- SHATI 2 NA TAI 1
- SURUALI (SHAMBA DRESS) 1
- TISHET 2
- SWETA 1
- TRACKSUIT 1
- BLANKET 1
- SHUKA 2
- SOKSI 2
- NEMBO 1

**WASICHANA**

- SKETI 2
- SHUKA 2
- BLANKET 1
- SHATI 2 TAI 1
- SKETI YA SOLO (SHAMBA DRESS) 1
- TISHETI 2
- SURUALI 1
- SOKSI 2

- SWETA 1
- TRACKSUIT 1
- NEMBO 1

**AKAUNTI NAMBA ZA SHULE KWA AJILI YA ADA TU.**

1. **CRDB Ac No. 01J1035987600**
   **A/C Name: Winning spirit Secondary School**

2. **LIPA KWA M-PESA Namba 5770686 WAKALA WINNING SPIRIT SEC**

**AKAUNTI YA UNIFORM NA MICHANGO MINGINE NI:-**
**NMB A/C No. 42810002124**
**A/C Name: Winning spirit Secondary School**

4. **AZANIA BANK ACC. No: 010000053263**
   **A/C Name: Winning Spirit high school**

- Ada iliyokwisha lipwa **<u>HAIRUDISHWI</u>** iwapo mwanafunzi ataamua kuacha au kufukuzwa shule.

**<u>NB</u>: M - PESA ya shule itumike kwa dharura tu na kwa idhini kutoka kwa meneja vinginevyo ada na michango yote hulipwa benki.**

1. **MAVAZI MENGINE - MWANAFUNZI AJINUNULIE**.

- Viatu - vyeusi vya kamba
- Raba za michezo, ndala za kuogea

**<u>NB</u>**: Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani akiwa shuleni bali atavaa sare za shule. Wakati wa madarasa na shamba dress baada ya masomo na siku za jumamosi na jumapili
(week-end).

**3. VIFAA VYA LAZIMA**.

(i) Kila mwanafunzi aje na karatasi (ream 5) A4 plain, na rulled paper 5, kwa ajili ya majaribio ya kila mwisho wa mwezi.

(ii) Darasani kila mwanafunzi atapaswa kujinunulia daftari, kalamu, na vifaa vya mahesabu.

(iii) Kila mwanafunzi wa bweni, aje na godoro la kulalia inchi tatu (3) futi mbili na nusu (2.5) si chini au zaidi ya hapo vinginevyo atarudishwa nalo.

(iv) Awe na sanduku la bati lenye kufuli.
(v) Mathematical set 1 ***(Yenye vifaa vyote)***
(vi) Counter Book **11** zenye ukubwa wa ***(Quire II or Quire III or Quire IV)***
(vii) Graph paper bando 1
(viii) Four figure 1 ***(Mathematics table)***
(ix) Dictionary 1
(x) Kamusi ya Kiswahili sanifu 1

**4. VIFAA VYA CHAKULA**

Kila mwanafunzi anatakiwa aje na Sahani, kijiko na kikombe. Hivi ni kwa ajili ya matumizi ya chakula hivyo atawajibika kuvitunza mwenyewe. (Sahani na kikombe visiwe vya plastiki)

**5. VIFAA VINGINE**

a) Unatakiwa uje na ndoo ya plastiki ndogo kwa ajili ya kuogea.
b) Picha nne (4) za passport size.
c) Rubber (squeezer na brush ) hard broom
d) Faili la kutunza mitihani yake.
e) Vitabu vya ziada na kiada.
f) Toilet paper dozen 1
g) Jembe 1 na fyekeo 1

**6. KUTEMBELEA MTOTO SHULENI NA MKUTANO WA WAZAZI.**

Kuwatembelea wanafunzi wazazi watajulishwa kabla ya siku 21

- Wanafunzi wa kidato cha pili na cha nne watalazimika kubaki shuleni likizo zote ili kufundishwa na Mzazi atamlipia gharama ya shilingi **250,000**/= kwa likizo ya mwezi wa sita, na shilingi **150,000**/= kwa likizo ya mwezi wa tisa ili kumwendeleza mwanafunzi kimasomo.

**NB: Fedha hizo zitalipwa kwa awamu mbili tu.**

**RATIBA YA SHULE**:

Inaanza saa 11:00 alfajiri hadi saa 04:00 usiku kwa siku za jumatatu hadi ijumaa. Siku za Jumamosi ni saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 usiku.

Mwanafunzi akikosa shule siku tatu mfululizo bila taarifa kamili inayokubalika atarudishwa nyumbani kwa kipindi kisichopungua siku Saba na baada ya hapo atakuja na Mzazi au Mlezi. Mwanafunzi akitoroka shule atakuwa amejiondoa shuleni mwenyewe.

**N.B**: Wanafunzi Hawaruhusiwi kwenda kusali nje ya shule badala yake watasali na
Kuendesha misa hapa shuleni kulingana na madhehebu na imani zao kwa siku za ibada,
Na kwa kufuata utaratibu maalum uliopangwa na shule.

Mwanafunzi akikamatwa na simu atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe

**MAZINGIRA YA SHULE**

Mazingira ni mazuri na ya kuvutia kwa utoaji na upokeaji taaluma, kuna umeme, maji na usafiri wa kuaminika kila wakati.

**CHAKULA MAALUM:**

Shule inatoa chakula bora kwa wanafunzi wote

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
P.O.BOX 11064,ARUSHA,TANZANIA
MKUU WA SHULE

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
MANAGER
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
MENEJA WA SHULE

# WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL

| Namba ya usajili wa shule: S. 3560 |
|---|

| Namba ya usajili wa mitihani S. 4014 |
|---|

P.O.BOX 11064
ARUSHA – TANZANIA
Executive Chairman: +255754 – 42104
Managing Director: +255754 – 381844
School Director: +255754 - 646446
HOS phone: +255766 - 657959
Bursar phone: +255745 - 6579-59
Email:winningspirit547@yahoo.com
info@winningspirithighschool.com
www.winningspirithighschool.com

| WEKA PICHA YA MWANAFUNZI HAPA |
|---|

**FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA SHULE**
**MWAKA 2026/2027**

**1. MAELEZO BINAFSI YANAYOHUSU MWANAFUNZI ANAYEOMBA NAFASI**

a) Jina la Mwanafunzi (kwa herufi kubwa) ____________________________________________
b) Jina la Mzazi / Mlezi ____________________________________________________
c) Tarehe ya kuzaliwa ____________________________________________________
d) Dini ________________________________________________________________
e) Kijiji alichozaliwa ____________________________________________________
f) Kata aliyozaliwa ______________________________________________________
g) Tarafa aliyozaliwa ____________________________________________________
h) Wilaya aliyozaliwa ____________________________________________________
i) Taifa _______________________________________________________________
j) Shule ya Msingi aliyosoma ____________________________________________
k) Shule ya sekondari aliyowahi kusoma_______________________________________
l) Kidato unachoomba kuingia/kuhamia_______________________________________
m) Sahihi ya Afisa Mtendaji wa kijiji chako. Kuthibisha picha na maelezo ya mwanafunzi. Picha ipigwe muhuri wa Afisa Mtendaji na sahihi _______________Tarehe _______________
n) Namba ya simu Mzazi / Mlezi ___________________________________________

**2. <u>MAELEZO YANAYOHUSU MZAZI / MLEZI / MFADHILI</u>**

a) Jina (kwa herufi kubwa) _______________________________________________
b) Anwani ya mahali unapoishi ____________________________________________
c) Kazi yako ___________________________________________________________
d) Jina la Kijiji unachoishi ________________________________________________
e) Jina la Wilaya / Mkoa _________________________________________________
f) Taja jina la atakayehusika na ulipaji Karo ya shule. (Weka alama Vema (*Tick*) panapohusika)
   i. Mzazi ( )
   ii. Mlezi ( )
   iii. Mfadhili ( )

## A. ILANI

## A. SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI ANAYEOMBA SHULE

Mimi (jina Kamili) ____________________________________ nimesoma masharti yaliyoandikwa hapo juu na kuyafahamu. Nimeshauriwa na Mzazi / Mlezi wangu naye amekubali, nimesoma masharti kwa makini kuwa kama nitachaguliwa kuingia shule hii, niko tayari kuyatii masharti na kanuni zote zinazotolewa na Uongozi wa shule.

**Sahihi ya mkono wangu……………....……………………..Tarehe …………....………**

## B. IJAZWE NA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………….. Mzazi / Mlezi wa…………………………
Ambaye anaomba kujiunga na shule ya Sekondari Winning Spirit, nimesoma masharti yaliyoandikwa hapo juu na kukubali. Ninathibitisha kwamba ni mimi nitakayepaswa kumlipia, mwanafunzi huyo karo ya shule na malipo mengine bila kucheleweshwa (kuchelewa)

Sahihi yangu …………………………… Tarehe …………………………

## 4. NAFASI YA KUJAZWA NA OFISI

Huyu ..……………………….................…………Tarehe …………………………………
Amekubaliwa/ hajakubaliwa kujiunga na kidato cha ………………………………………..

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
P.O.BOX 11064,ARUSHA,TANZANIA
…………………………
MKUU WA SHULE

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
MANAGER
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
MENEJA WA SHULE

# WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL

## TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE

kila taasisi imejiwekea taratibu na sheria ambazo zinapaswa kufuatwa ili kufanikisha shughuli za kila siku na hatimaye kufikia malengo yaliyowekwa.

Zifuatazo ni taratibu za shule ya Sekondari Winning Spirit, ambazo kila mwanafunzi anayejiunga na shule hiii anapaswa kuzifuata kikamilifu.

### A. TARATIBU ZA SHULE

**1. Kuwahi shuleni/darasani**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwahi darasani kila siku sawasawa na ratiba iliyopangwa. Likizo

inapokwisha, wanafunzi wa bweni wanatakiwa kuripoti shuleni siku na saa iliyopangwa.

Mwanafunzi aje na mahitaji yake yote (yaliyoidhinishwa) akishariporti hataruhusiwa kutoka wala kwenda nyumbani.

Mwisho wa kuripoti shuleni ni saa kumi na nusu jioni (10:30) baada ya hapo hakuna mwanafunzi atakayepokelewa. Akija atarudishwa alikotoka na shule haitahusika na lawama zozote.

Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti atapewa adhabu au kurudishwa nyumbani, kuendana na siku alizokosa masomo.

**2. Taaluma**

**Wastani wa shule ni asilimia (60%)**

Hivyo ili kujiunga na shule hii, na ili kuvuka kidato kimoja kwenda kingine ni lazima uwe na wastani huo (60%) na pamoja na kufikia wastani( 60%) ni lazima mwanafunzi awe na ufaulu wa daraja la kwanza ( Division one).

Ili kufanikisha hili ni lazima mwanafunzi ajitume, ahudhurie vipindi vyote vya darasani, ajiwekee ratiba binafsi ya kujisomea aidha maktaba, maabara au katika mazingira mengine yaliyokubaliwa ndani ya shule (ajiwekee malengo ya kufaulu bila kusukumwa).

**3. Heshima na utii**

Ni wajibu wa mwanafunzi kufanya yafuatayo:-

- Kuheshimu jamii nzima ndani na nje ya shule.
- Kuheshimu bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
- Kutii wito utakaotolewa kwa kengele, ishara, sauti n.k na kuwahi panapohusika.
- Kujiheshimu yeye mwenyewe kwa kuvaa vema, kuongea lugha stahiki kwa watu tofauti tofauti katika jamii.

4. **Usafi na uwajibikaji**

Ni wajibu wa mwanafunzi kuwa msafi yeye mwenyewe, mavazi yake, malazi yake, chumba chake, vyombo vyake na kujituma kufanya usafi, kuokota uchafu kwenye mazingira mbalimbali ya shule, nywele zikatwe vema bila mitindo au kupakwa kemikali ya aina yoyote.

Kutunza vifaa vyote vya shule kwa uaminifu. Endapo utasababisha uharibifu wa mali za shule basi utawajibika kulipa gharama.

Mwanafunzi atawajibika kufanya shughuli nyinginezo kwa ustawi wa shule na jamii kwa ujumla. Kama kulima bustani za maua, mbogamboga na miradi mingine ya shule. (kuelimika ni pamoja na kufanya kazi za mikono).

5. **Lugha**

   Lugha rasmi ya mawasiliano shuleni ni kiingereza. Hivyo mwanafunzi atatakiwa kutumia lugha hii wakati wote. Hairuhusiwi kugonga kengele hovyo, kupiga kelele au kutoa sauti zitakazo haribu utulivu wa shule.

6. **Wageni**

   Wanafunzi wanaruhusiwa kutembelewa mara moja tu kwa muhula. Nayo ni jumamosi ya pili ya mwezi wan ne na mwezi wa kumi au itakapotokea dharula.

   Ikiwa kuna tatizo linalomhitaji mzazi/Mlezi, shule itafanya mawasiliano na si mwanafunzi.

   Mwanafunzi haruhusiwi kumualika mgeni yeyote shuleni au kumuita Mzazi/Mlezi shuleni bila ruhusa ya Mkuu wa shule.

   Wageni wote wa wanafunzi watapokelewa na Mlezi (Matron) wa shule. Hairuhusiwi kuletewa chakula au kinywaji cha aina yoyote.

**B. SHERIA ZA SHULE**

i. Kuwa katika sare ya shule daima, safari zote za nje ya shule, sare rasmi za shule zivaliwe, wakati wa kufunga na kufungua shule, wanafunzi wote wawe katika sare rasmi.
ii. Kutoka nje ya eneo la shule, kwa sababu yoyote ile, ni kwa kibali cha Mkuu wa shule tu.
iii. Vifaa vifuavyo haviruhusiwi mwanafunzi kuwa navyo shuleni:- simu, pasi, heater, radio, line za simu, album za picha, vito vya thamani, rangi za kucha, visu na mishumaa.
iv. Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia chumbani au nyumbani kwa mfanyakazi yeyoote, ofisini au jikoni bila kibali maalum.
v. Hairuhusiwi wanafunzi kukusanyika, kufanya kikao au mkutano wowote nje ya ratiba au bila kibali cha Mkuu wa shule.
vi. Mwanafunzi haruhusiwi kumwingiza mgeni yeyote bwenini, wala kuingiza kinywaji au chakula chochote bwenini.
vii. Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kujipamba mfano kutinda nyusi, kupaka wanja, kuvaa bangili, hereni, pete, cheni n.k.
viii. Hairuhusiwi kujihusisha na vitendo vyovyote vya kimapenzi ndani au nje ya shule
ix. Mwanafunzi haruhusiwi kulala bwenini bila ruhusa ya mwalimu wa zamu au matron (hata kama ni mgonjwa).
x. Ni lazima mwanafunzi kufanya majaribio na mitihani yote inayotolewa shuleni nyakati zote.
xi. Kubadilisha kwa namna yoyote sare za shule bila ruhusa ya maandishi toka kwa mwalimu wa malezi au matroni.

**C. ADHABU**

Adhabu zitakazotolewa kwa kuvunja sheria au kukiuka taratibu zilizoanishwa ni pamoja na:-

- Kumwita Mzazi/Mlezi shuleni na kupewa onyo.
- Kusimamishwa masomo kwa siku 7,14,21 au 28 kuendana na kosa.
- Kufanya kazi za mikono kama usafi, kufyeka, kulima n.k
- Kulipa gharama za uharibifu na kulipia gharama ya kuita bodi ya shule.
- Kuandika idadi kubwa ya maneno (ya somo lolote), kutunga sentensi nyingi, kutunga maswali mengi au adhabu yoyote ya kitaaluma itakayotelewa na mwalimu wa somo husika.
- Kufukuzwa shule.

**D. MAKOSA YAFUATAYO ADHABU YAKE NI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.**
**(Hakuna mjadala wala kikao chochote).**

- Makosa ya jinai. Mf. Kupigana, wizi, kutishia n.k.
- Kupata mimba, kusababisha mimba, kutoa mimba, viendo vya uasherati ndani au nje ya shule, mahusiano ya kimapenzi.
- Kutoroka shule/kuruka ukuta.
- Kukataa adhabu ya mwalimu yeyote.
- Unywaji pombe, uvutaji sigara, madawa ya kulevya.
- Kugoma, kuchochea mgomo, kuandamana, kufanya mikutano isiyo na kibali.
- Kumiliki au kukutwa na simu au laini za simu.
- Kuhusishwa katika kesi au kushtakiwa mahakamani nje ya shule
- Kuharibu kwa makusudi mali ya shule.
- Kupiga simu nyumbani, kuandika ujumbe au kuwasiliana na mtu yeyote nje ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.

Pamoja na sheria hizi, ni vyema mwanafunzi akatambua kuwa siku zake za masomo zimewekwa kwa idadi, hivyo kufanya makosa na kupewa adhabu ni kupoteza muda wake wa kusoma.

Tunasisitiza kuwa ni lazima mwanafunzi kuishi shuleni kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa ili kuishi shuleni kwa utulivu na kutumia muda wote katika masomo kama ilivyopangwa.

Hivyo ni wajibu wa wazazi na walezi kuwafundisha watoto wao kuishi shuleni kwa uadilifu na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
P.O.BOX 11064,ARUSHA,TANZANIA
MKUU WA SHULE

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
MANAGER
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
MENEJA WA SHULE

# WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL

## FOMU YA KUKIRI KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

**Ukiri wa Mwanafunzi:**

Mimi ______________________________, ninakubali nafasi hii niliyopata ya kujiunga na shule hii ya Winning Spirit. Nimezisoma sheria na taratibu zake na nimezilewa.

Hapa ninaahidi kuwa nitafuata sheria na taratibu zote zilizowekwa.

Sahihi ya Mwanafunzi _____________ tarehe_________________

**Ukiri wa Mzazi/Mlezi**

Mimi ________________________________________________ ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ____________________________________ Ninakubali ajiunge na shule hii ya Winning Spirit. Ninaahidi kutoa ushirikiano kwa mwanangu na kwa shule ili kumlea katika maadili yanayopasa na kuhakikisha kuwa ninamsaidia afikie lengo lililowekwa ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vikao vya wazazi, kufuatilia taaluma yake, kulipa ada kwa wakati, kuhakikisha mwanangu yuko salama awapo likizo na kuhakikisha anarudi shuleni kwa tarehe na saa iliyopangwa.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi _____________________ tarehe___________________

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
HEAD OF SCHOOL
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
P.O.BOX 11064,ARUSHA,TANZANIA
MKUU WA SHULE

WINNING SPIRIT HIGH SCHOOL
MANAGER
12 JUN 2025
TIN: 106 - 214 - 468
MENEJA WA SHULE

## MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE WINNING SPIRIT SECONDARY SCHOOL MEDICAL EXAMINATION FORM

**To be completed by Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Winning Spirit Secondary School.**

**Full name:…………………………………………………………......…Age……………..**

1. "AIDS" Test …………………………………………………………………………....
2. Blood count (Red and white) ……………………………………………………………….
3. Urine Examination ………….…………. Stoll Examination……………………………….
4. Syphilis Test ……………………………………………………………………………...
5. T.B test …………………………..…………Ear Test ……………..………………………..
6. Spleen …………………………………………………………………………………….
7. Abdomen ………………………………………………………………………………….
8. Additional information or any other physical mental hereditary of infectious Diseases
   ………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………

Treatment after Examination ………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
(Please state nature of treatment)

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further education.

Signature …………………………………………

Designation……………………………………….

Station ……………………………………………

**Date:……………………………………    Official stamp………………………………**

**<u>N.B</u>**: Sehemu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali ya Serikalli Wilaya / Mkoa.